

IGUNGA YA MAENDELEO



**DC atoa salamu za Serikali kwenye
Baraza la Madiwani Igunga**



Maelekezo kutoka kwa viongozi wetu wakuu wakiongozwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha tunasimamia na tunabuni vyanzo vipyta vya mapato na kusimamia mianya yote ya upotevu wa mapato ili kuweza

kufika lengo la makusanyo kama mpango na bajeti ya serikali ya mwaka 2022/2023 iliyopitishwa na bunge la Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Pia Mhe Sauda Mtondoo mkuu wa wilaya ya Igunga alisema Mwaka huu 2022 ni mwaka wa Sensa kitaifa

;sisi sote kwa nafasi zetu, kama viongozi wa Kisiasa tunatakakiwa kwenda kuhamasisha wananchi ili kujitokeza na kutoa ushirikiano kwa makarani wa Sensa ambaao wataanza kuhesabu watu siku ya Jumanne ijayo tarehe 23/8/2022.

HALIUZWI



Limeandaliwa na Ramadhan Salum



TANESCO mradi wa REA awamu ya III mzunguko wa I

Mradi huu umenufaisha jumla ya vijiji 26 katika wilaya ya Igunga. Mradi huu umehusisha ujenzi wa njia kubwa ya umeme yeye urefu wa km 114.943, ujenzi wa njia ndogo yeye urefu wa km 101.971, ufungaji wa transfoma 41 na uunganishaji wa wateja wapya 1421. Utekeleza wa mradi huu unafanywa na mkanadarasi JV-POMY, OCTOPUS na INTERCITY. Gharama ya mradi ni takribani TZS 3 billion saba nukta moja.

(Alisema Eng. Godfrey Vomo wakati akisoma taarifa yake mbele ya baraza la madiwani 17/8/2022). Eng. Vomo aliendelea kueleza kuwa mradi wa REA awamu ya III mzunguko wa II, katika awamu hii jumla ya vijiji 60 vitanufaika na umeme. Awamu hii itahusisha ujenzi wa njia kubwa ya umeme yeye urefu wa km 494.4, ujenzi wa njia ndogo yeye urefu wa km 60, ufungaji wa transfoma 60 na uunganishaji wa



wateja wapya 1188. Utekeleza wa mradi huu una-fanywa na mkanadarasi M/s CYLEX. Kwa gharama ya mradi ni TZS 34,431,973,192.06. (Gharama hizi ni pamoja na wilaya ya Sikonge, Urambo na Kaliua).

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. (RUWASA)



Mamlaka inaendelea na kutoa huduma ya maji viji-

jini, pia inaendelea na upanuzi wa mradi wa eneo la Matinje, maji ya Ziwa victoria kutoka Ibologero, kwenda matinje. Uchimbani wa mtaro, ulazaji uungan-

ishaji na ufungaji bomba umbali wa km 15.713, ume-

fanyika, na Ujenzi wa vituo 6 vya kuchotea Maji umefanyaika, wananchi wanapata huduma. Ameyasema hayo Fundi Mkuu Bw: Harubu, kaimu meneja RUWASA, kwenye Baraza la Madiwani Ukumbi wa Halmashauri ya wilaya Igunga 17/8/2022.



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Igunga. (IGUWASA)



Eng; Bakari Mohamed, kaimu Mkurugenzi mtendaji

IGUWASA, amesema, pamoja na kutoa huduma ya maji Igunga mjini bado wanaendelea na upanuzi wa mtandao wa huduma ya majisafi na salama katika vijiji vya Mwabakima, Jogohya na Mwamashimba. Upanuzi huo ulianza Desemba 06 2021 na utakamilika Septemba 06 2022. Makadilio ya gharama za kutekeleza mradi huu ni takribani TZS million mia Nane thelathini laki saba na elfu sita tisini na tano na senti tano. (830,706,695.50). Eng. Mohamed pia alilieleza baraza la madiwani kuwa mradi ukikamilika, Takribani wanakijiji elfu kumi mia nne thelathini na moja (10,431) watanufaika na huduma ya majisafi na salama. Kwasasa umefikia asilimia 78% za utekelezaji.

Mhe; Regina Dotto Thadeo, mwenyekiti wa CCM wilaya, atoa salamu kwenye baraza la madiwani



Pamoja na salamu, mwenyekiti alimalizia kusema kwamba "Atakae kwamisha zoezi la Sensa achukuliwe hatua za kisheria CCM haitamvumilia mtu atakaevuluga zoezi hili"



Idara ya Elimu msingi ya kabidhi madawati 29/7/2022, yaliotolewa na Mhe Mkuu wa Mkoa Tabora kama pongezi kwa wilaya ya Igunga kwa ufaulu mzuri Mtihani wa Taifa 2022. Kulia ni Afisa Elimu msingi Bi. Dora simbachawene na Kushoto ni Bw; Joseph Elias Kaimu mkurugenzi.



Mapato Igunga yaongezeka 2021/2022

Kwa kipindi cha mwezi wa Aprili Halmashauri imekusanya kiasi cha TZS 2,564,886,380.00 sawa na asilimia 85.6 ya makadirio ya mapato ya mwezi Aprili yaani 2,995,387,523.1.Kwa Mhutasari wa taarifa ya

Mapato mwezi Julai 2021 hadi Aprili 2022,1. Vyanzo vya mapato ya ndani 3,206,768,495.50. 2 Ruzuku 20,212,337,332.94.3.Miradi ya maendeleo 7,591,077,840.00.4. Wahisani 1,292,875,452.45.

Jumla ya mapato ni 32,303,059,120.89.Mafanikio haya makubwa yanatokana na ushirikiano baina ya Madiwani (Kamati ya Fedha) na Wataalamu wa Halmashauri.



IGUNGA YA MAENDELEO



uk 5

Mheshimiwa Lightness Solomon Kahuta, Hakimu Mkazi awaapisha Makarani katika ukumbi wa Accacia land 15/8/2022.



Makarani wa sensa kituo cha Accacia land wilayani Igunga waapishwa.



Mwalimu mkuu Hanihani, ashukuru uongozi wa Idara ya Elimu kwa kumpatia madawati 25. Mwl Joseph Luhenga Costantine, alitoa wito kwa Wadau wengine kuiga mfano wa EXIM BANK, kwakutoa madawati Hayo. Aidha Mwalimu mkuu huyo ameongeza kuwa uwepo wa madawati ya kutosha darasani kunapunguza utoro kwa wanafunzi na kuongeza ufaulu.



AKABIDHI MADAWATI 25. Kwa niaba ya Mkurugenzi mtendaji Bw Joseph Elias amkabidhi madawati 25 Mwalimu mkuu wa shule ya msingi Hanihani katika Ofisi ya Halmashauri 29/7/2022.



TARURA, matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, mpaka Juni 30/2022

Halmashauri ya wilaya Igunga ilitengewa kiasi cha TZS 965,230,993.71 kama fedha ya matengenezo ya barabara wilayani Igunga, hayo yamesemwa na Eng; Costantine S. Ibengwe katika baraza la madiwani Wilaya ya Igunga 17/8/2022. Eng: Ibengwe ameongeza kuwa, Halmashauri imepangiwa



kutumia TZS 1,000,000,000,(Bilion moja) ikiwa ni fedha ya matengenezo ya barabara kwa

mfuko wa majimbo ya Manonga na Igunga. Aidha Ibengwa amesema serikali ya mama Samia imeidhinisha bajeti ya nyongeza ya TZS 2,000,000,000,(Bilion mbili) kwa majimbo ya Igunga na Manonga kwa matengenezo ya barabara.

DC igunga awapongeza wote walio-fuzu mafunzo ya sensa.

Mhe; Sauda Mtondoo, Mkuu wa wilaya ya Igunga amewapongeza wanasesmina wote kwa kufaulu mitihani kwa wastani wa asilimia 81. Aidha amewataka Makarani wa Sensa kwenda kufanya kazi waliofundishwa kwa kufuata kanuni na taratibu na miongozo ya sensa. Mheshimiwa Mtundo, amesema takwimu sahihi utakazo zikusanya ndio msingi wa mipango ya

maendeleo kwa miaka 10 ijayo. Pia amewataka makarani kuhesabu watu wote na kila mtu ahesabiwe mara moja (1) tu, bila kuwa na kisingizio chochote kwa siku zilizopangwa. Mtundo alisisitiza kuwa kila aliyepata kazi ya sensa ni ajira ya muda mfupi, am-bayo inatumia miongozo ya utumishi wa umma. Ni

lazima kila karani kujitambulisha kwa viongozi wa



mitaa vijiji na vitongoji ili zoezi la sensa lifanikiwe. (Alisema mkuu wa wilaya.)

IGUNGA YA MAENDELEO



uk 7



Wakuu wa Idara na Vitengo waliopaisha Mapato Igunga, wakiongozwa na Bi. Fatuma O. Latu Mkurugenzi mtendaji wilaya ya Igunga.



Wakufunzi wa Makarani, IT na wasimamizi wa maudhui (Sensa) wakisikiliza hotuba ya Mhe;Mkuu wa wilaya 15/8/2022 katika ukumbi wa Shule ya msingi Accacia land.



Viongozi wa Chama cha mapinduzi wampongeza Mhe;Lois Azori Fumbuka, kwa kuchaguliwa tena kuwa makamu mwenyekiti wa Halmashauri. Kulia ni Mhe; Regina Dotto Thadeo Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya igunga, na kushoto ni Bi; Mwanamvua Kilo Katibu wa CCM wilaya Igunga



Waheshimiwa Madiwani wa wilaya ya Igunga wakati wa DUA, ya kuiombea Halmashauri kabla ya kuanza kikao cha Baraza la mwisho wa Mwaka wa fedha 2021/2022.

